



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na 126 cha Sheria ya Petroli Sura ya 392 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 6(1) ya Kanuni za Mafuta (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji wa Gesi Asilia) za mwaka 2018)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa miundombinu (bomba) la kusambaza gesi asilia lenye urefu wa kilomita 2 kutoka **SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI (TPDC)**. Mradi huu ni kwa ajili ya kuunganisha kiwanda cha *Sapphire Float Glass Limited* kwenye mtandao wa kusambaza gesi asilia wa TPDC uliopo Mkuranga. Bomba hili litajengwa katika Kijiji cha Mkiu, kata ya Nyamato katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Bomba hili litapita kando ya barabara ya Kilwa (Kongowe-Marandego) umbali wa kilomita 1.7 na kuingia eneo la kiwanda umbali wa kilomita 0.3.

Hivyo basi, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, awasilishe maoni au pingamizi kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**  
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**  
**S. L. P 2857, Dodoma.**

Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;

Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

**Imetolea na:**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**EWURA**